

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

S.L.P. 35091 ♦ DAR ES SALAAM ♦ TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

MAADHIMISHO YA SABA YA WIKI YA UTAFITI NA UBUNIFU

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinapenda kuwataarifu na kuwaalika wadau na Watanzania wote kwa ujumla kushiriki katika **Maadhimisho ya Saba ya Wiki ya Utafiti na Ubunifu** ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yatakayoanza Jumanne tarehe 24 Mei hadi Alhamisi tarehe 26 Mei 2022 kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni katika eneo la Maktaba Mpya, Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere, Mlimani. Ufunguzi rasmi wa Maadhimisho haya utafanyika siku ya Jumanne tarehe 24 Mei 2022 katika Ukumbi wa Maktaba kuanzia saa 2.00 asubuhi, ambapo Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Kaulimbiu ya Maadhimisho haya ya Saba ya Wiki ya Utafiti na Ubunifu ni **Utafiti na Ubunifu kwa Manufaa ya Kijamii Nchini Tanzania**.

Aidha, katika siku hii ya ufunguzi kutakuwa na Wazungumzaji Wakuu wawili amba ni mfanyakishara Ndugu Seif Ali Seif, Mkurugenzi Mkuu wa Superdoll Ltd ambaye atatoa mada kuhusu **Ushirikiano wa Sekta ya Uzalishaji na Vyo vya Elimu ya Juu nchini Tanzania**, na Profesa Evelyn Mbede, Profesa katika Sayansi ya Jiolojia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam atakayezungumzia **Gesi ya Helium na Maendeleo ya Viwanda Nchini Tanzania**.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitatumia fursa hii kujipambanua katika utafiti amba ni mojawapo ya majukumu yake makuu, kwa kuonesha shughuli zake za utafiti, ubunifu, huduma kwa jamii na ubadilishanaji maarifa kama njia ya kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii nchini hasa katika kufikia malengo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kukuza uchumi na hivyo kuboresha maisha ya wananchi.

Kati ya miradi ya utafiti na ubunifu zaidi ya mia tatu (300), mwaka huu Chuo kitaonesha miradi mia moja na mitatu (103) iliyofanya vyema zaidi kama vile mradi wa maabara ya kidijitali (off grid mobile universal digital laboratory); na glavi maizi kwa wenyewe matatizo ya kusikia na kuzungumza (Smart glove for the hearing and speech impaired); na mtambo maalumu wa kuyeyusha shaba kwa ajili ya wachimbaji wadogo nchini Tanzania (Smelter for Copper Extraction for Artisanal and Small Scale Miners (ASMs) in Tanzania).

Wiki hii pia hutoa fursa ya kuimarisha ushirikiano baina ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wadau mbalimbali kitaifa na kimataifa. Kwa kuzingatia hilo, siku ya pili ya maadhimisho, Jumatano tarehe 25 Mei 2022, kuanzia saa 2.00 asubuhi kutakuwa na **Mjadala Maalum wa Ushirikiano ya Kimkakati** utakaowashirikisha wadau kutoka

katika sekta binafsi na za umma pamoja na waandishi wa habari. Mjadala huu utajikita katika masuala ya viwanda, biashara, ujasiriamali, ubunifu na utafiti.

Wiki hii ya Maadhimisho ya Utafiti na Ubunifu itatumika pia kutambua michango iliyotukuka ya wanataaluma na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika utafiti, ubunifu na ubadilishanaji wa maarifa. Hivyo, katika sherehe za kufunga Maadhimisho ya Wiki ya Maadhimisho haya tarehe 26 Mei 2022, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Profesa Adolf Faustin Mkenda (Mb.) atawatunuku tuzo watafiti na wabunifu bora katika makundi yafuatayo:

1. Mradi Bora wa utafiti.
2. Vitengo/Idara Zilizoingiza Kiasi Kikubwa cha Fedha za Utafiti.
3. Vitengo/Idara Zilizoingiza Kiasi Kikubwa cha Fedha za Ubunifu.
4. Watafiti Walioingiza Kiasi Kikubwa cha Fedha za Utafiti.
5. Mtafiti Bora.
6. Mbunifu Bora.
7. Miradi Bora ya Wanafunzi wa Uzamili.
8. Miradi Bora wa Wanafunzi wa Shahada za Awali.
9. Mradi Bora wa katika Kutoa Huduma kwa Umma.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawaalika wadau wote wa elimu, Jumuiya ya Wahitimu, Viongozi wa Serikali, wadau wa maendeleo, mabalozi, viongozi wa kisiasa, viongozi wa vyama vya kiraia, waandishi wa habari na wananchi wote kwa ujumla kushiriki katika Maadhimisho ya Saba ya Wiki ya Utafiti na Ubunifu 2022 ambayo ni muhimu sana katika kuleta chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.

Imetolewa na:

**Prof. William A. L. Anangisye
MAKAMU MKUU WA CHUO
18 MEI 2022**